



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb: Na. CHAL/LD/2583/ARR

31.07.2023

Mkurugenzi Mkuu,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

**YAH: KIWANJA NAMBA 11 KITALU " B" VIGWAZA CHALINZE (CT
NO.11216PWN).**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Napenda kukujulisha kuwa tulipokea nyaraka za uhamisho wa milki za kiwanja tajwa hapo juu kutoka kwa ndugu **Athuman Omary Said** wa S.L.P 3029 Kibaha hapa nilimrejea kama mmilikaji wa kiwanja tajwa kwenda kwa kampuni ijulikanayo "**UNION MEAT ABATTOIRS LIMITED of P.O.Box 9104 DAR ES SALAAM**" hapa nikiirejea kama Kampuni ya kigeni; na baadhi ya nyaraka muhimu zilizowasilishwa ni pamoja na mkataba wa mauziano, Land Form No 35, 30 na 29, nakala za "Passports" za kusafiria za wakurugenzi wa kampuni UNION MEAT ABATTOIRS LIMITED (nakala mbili zilizothibitishwa kama nakala halisi), "Annual returns", "Memorandum and Articles of Association", "Certificate of incorporation" (nakala mbili zilizothibitishwa kama nakala halisi), Cheti cha usajili wa Kampuni (certificate of registration), "Business licence" na "TIN number"

Aidha nakujulisha kuwa kampuni ya "**UNION MEAT ABATTOIRS LIMITED**" haikuwasilisha "Certificate of incentive" ya kiwanja hiki kwa ajili ya uwekezaji hivyo nawaleta kwako ili uwe katika nafasi nzuri ya kupitia nyaraka zao na kuwapatia nyaraka hiyo (Certificate of Incentive) kwa hatua zaidi za ushughulikiaji wa maombi yaliyowasilishwa.

Naomba kuwasilisha.


Ramadhani Possi
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHALINZE**



NAKALA:-

1. Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
Mkoa wa Pwani,
1 MTAA WA ARDHI,
S. L. P 9230,
11477, DAR ES SALAAM – (Kwa taarifa na ushauri)
2. Athumani Omary Said,
S.L.P 3029,
KIBAHA- PWANI (Kwa taarifa na ufuatiliaji)
3. Mkurugenzi,
UNION MEAT ABATTOIRS LIMITED
S.L. P 9104,

DAR ES SALAAM (Kwa taarifa na ufuatiliaji wa "Certificate of Incentive TIC" ya kiwanja hiki).